

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZAMITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHU
MKOA WA DODOMA

Simu: +255 26 2961400
Nukushi.: +255 26 2961401
Barua Pepe: info@bahidc.go.tz
ded@bahidc.go.tz
Tovuti: www.bahidc.go.tz



Msimamizi wa Uchaguzi,
S. L. P. 2993,
Dodoma,
TANZANIA.

TANGAZO KWA UMMA KUHUSU UKOMO WA KUWA MADARAKANI KWA WENYEVITI WA VIJJI, MITAA, VITONGOJI NA WAJUMBE WA SERIKALI ZA MITAA

Kama ilivyotangazwa katika tangazo la **Serikali Na. 371** kwa mujibu wa **Kanuni ya 22** za Kanuni za Uchaguzi wa Mamlaka za Miji midogo, pamoja na Tangazo la Serikali Na.373 la mwaka 2019 na kwa Mujibu wa **Kanuni ya 22** ya Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa kitongoji katika Mamlaka za Wilaya za Mwaka 2019.

Ninawataarifu kuwa **Kuanzia tarehe 22/10/2019** ndiyo Ukomo wa kuwa Madarakani kwa Viongozi wote wa Halmashauri za Vijiji vyote vya Halmashauri ya Wilaya ya Bahi ambao ni;

- 1).Mwenyekiti wa Kijiji
- 2).Mwenyekiti wa Kitongoji
- 3).Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji

Hivyo Majukumu, shughuli na Majukumu yao yatatekelezwa na Wataalam waliopo Katika maeneo ya Vijiji mpaka hapo taratibu za upatikanaji wa Viongozi wapya zitakapokamilika.

Hivyo basi Wananchi wote mnajulishwa kuwa hakutakuwa na Nyaraka yoyote au huduma yoyote itakayotambulika Kisheria ikiwa itatolewa na Viongozi/Kiongozi wa ngazi hizo kuanzia tarehe 22/10/2019 huduma zote zitatolewa na Afisa Mtendaji wa Kijiji husika hadi pale Uchaguzi wa Viongozi utakapokamilika tarehe 24/11/2019

"VIONGOZI BORA WA SERIKALI ZA MITAA NI CHACHU YA MAENDELEO. NI HAKI NA WAJIBU WAKO KUJIANDIKISHA, KUGOMBEA NA KUCHAGUA VIONGOZI BORA"

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA;

Charles A. Mduma

MSIMAMIZI WA UCHAGUZI

BAHI

